# UJENZI WA BANDA AU NYUMBA YA NGURUWE

**Na Augustino Chengula**

## 1. Uchaguzi wa eneo la kujenga banda

Mambo muhimu ya kuzingatia wakati unapendekeza eneo la kujenga banda au nyumba ya nguruwe

i. Liwe ni eneo lililo kwenye mwinuko japo kidogo kiasi cha kutotuamisha maji ya mvua
ii. Ni vizuri eneo likawa na kivuli cha miti ya asili au kupandwa na liwe na uwezo wa kupitisha hewa ya kutosha
iii. Ni vizuri likawa mbali kidogo na makazi ya watu hasa kama unataka kufuga nguruwe wengi.
iv. Pia kama unataka kufuga nguruwe wengi, ni vizuri eneo likawa karibu na barabara au liwe linafikika kwa gari ili iwe rahisi kusafirisha nguruwe wako wakati wa kufanya biashara.
v. Upatikanaji wa maji na umeme uwe wa uhakika

## 2. Mpango wa ujenzi wa banda au nyumba nzuri wa nguruwe


Mambo ya muhimu kwenye nyumba ya nguruwe ni kama ifuatavyo;

i. Sakafu ya nyumba lazima iwe ya mita 3 kwa 3
ii. Sakafu ya nyumba lazima iinuke sentimita 60 juu ya ardhi
iii. Paa lazima liwe na uwezo wa kuzuia mvua kwa asilimia 100
iv. Upande mmoja wa paa lazima uinuke zaidi ya mwingine, ule upande mrefu zaidi utazame mwelekeo usio wa jua ili kukinga mwanga makli wa jua. Lakini hakikisha kuwa mwanga wa wa jua unaingia ndani ya banda na kivuri kipo upande mmojawapo.
v. Banda au nyumba ijengwe kwa uimara wa kutosha, lakini ni vizuri kutumia vifaa vinavyopatikana katika eneo husika kwa bei rahisi. Banda au nyumba ijengwe kwa kuzingatia aina ya ufugaji na hali ya hewa ya mahali husika.
vi. Banda au nyumba ya nguruwe ni vema ikawa yenye kuleta furaha kwa nguruwe na si mateso; iwe na hewa nzuri, kivuri cha kutosha, isiyo na unyevunyevu, joto kali, harufu mbaya wala matope.
vii. Banda au jingo lijengwe kwa urefu unaotazama Mashariki-Magharibi ili kukinga jua na mvua.
viii. Banda au nyumba ya nguruwe igawanywe katika maeneo madogo madogo (pens) yatakayoweka nguruwe kulinga na umri wao wa kuzaliwa. Namba na idadi na ukubwa wa vyumba utategemea na namba ya nguruwe inayotarajiwa kuwekwa au kuzaliwa katika uzazi husika.

ix. Gharama za ujenzi wa banda au nyumba ya nguruwe zitegemeane sana na aina ya uzalishaji unaotarajia kuufanya ili uzalishaji uweze kuwa wenye tija.

3. **Aina za sakafu**

Kimsingi, kuna aina kuu tatu za sakafu zinazotumiwa na wafugaji wa nguruwe sehemu mbalimbali duniani kama inavyoonekana kwenye picha hapa chini:




4. **Mahitaji ya nafasi kwa nguruwe**

Mahitaji ya nafasi katika ya nguruwe katika banda au nyumba ya nguruwe inategemea na aina ya nguwruwe walioko kwenye nyumba ya nguruwe.

***i. Nguruwe wadogo***

Hawa ni nguruwe walioachishwa kunyonya, wana hitaji mita za eneo la mraba kuanzia 0.3 hadi 0.5 kwa kila kitoto kimoja cha nguruwe. Hivyo ili kujua ukubwa wa chumba (pen) cha kukaa vitoto hivyo zidisha hiyo namba na idadi ya vitoto vya nguruwe unaotaka kuwaweka.



**Picha:** Mfano mzuri wa banda la vitoto vya nguruwe lenye nafasi ya kukidhi mahitaji wa nguruwe.

-Sakafu ya banda au nyumba ya nguruwe ijengwe kwa simenti au kwa udongo mgumu lakini isiwe ya kuteleza. Sakafu pia iwe na mteremko mdogo kurahisha usafishaji na maji na kuruhu sakafu kukauka kwa haraka na isiwe na mibonyeo yeyote.

***ii. Nguruwe dume:***

Nguruwe dume kwa ajili ya kuzalisha wanahitaji nafasi ya eneo la mraba kati ya mita 6 hadi 8.



-Uangalizi mkubwa kwa nguwe dume unahitajika maana anaweza kutoka ndani ya banda na kufuata majike hasa yaliyoko kwenye joto (majike yaliyotayari kwa kupandwa).

***iii. Nguruwe wenye mimba***


Nguruwe wenye mimba wanahitaji nafasi kati ya mita 1.5 hadi 2.0 za eneo la mraba kwa kila nguruwe mmoja.




Nguruwe wenye mimba wanahitaji mazingira yenye utulivu sana. Wakati mwingine nguruwe mwenye mimba anahitaji chumba cha peke yake. Katika mazingira ya joto ni vizuri kuweka angalau nguruwe wasiozidi watatu kwa chumba kimoja.

### *iv. Nguruwe wanaonyonyesha*


Nguruwe wanaonyonyesha wanahitaji nafasi kati ya mita 4 hadi 6 za eneo la mraba kwa kila nguruwe.



Nguruwe wanaonyonyesha pia wanahitaji mazingira tulivu, hivyo wanapaswa wapewe chumba cha peke yao. Chumba chao kinahitaji kiwe na vitu vifuatavyo; sehemu ya kuzalia, vifaa vya kutoa na kupunguza joto, kiota/chumba cha nguruwe wadogo, chombo cha chakula cha watoto na chakula cha mwanzo cha watoto.



Banda la kuzalia



Taa ya kuongeza joto



Chombo cha chakula cha watoto



Kiota/chumba cha watoto

### *v. Nguruwe wa Kunenepeshwa*


Nguruwe wa kunenepeshwa wanahitaji nafasi kati ya mita 0.5 hadi 1.0 eneo la mraba kwa kila nguruwe.




-Sakafu ya banda au nyumba ya nguruwe ijengwe kwa simenti au kwa udongo mgumu lakini isiwe ya kuteleza. Sakafu pia iwe na mteremko mdogo kurahisha usafishaji na maji na kuruhu sakafu kukauka kwa haraka na isiwe na mibonyeo yeyote

5. **Aina mbalimbali za nyumba na au mabanda ya nguruwe**

Zipo aina mbalimbali za nyumba na au mabanda ya nguruwe yanayotumika sehemu mbalimbali duniani na hasa maeneo ya vijijini. Mifano ya nyumba au mabanda unazoweza kujenga ni kama inavyoonyesha kwenye michoro hapa chini:





Jua
Nzuri, ina kivuri

Jua
Sio nzuri, hakuna kivuri





6. **Vyombo vya chakula**

Chombo cha chakula lazima kishikiliwe vizuri kwenye sakafu ili nguruwe wasikiyumbishe na kumwaga chakula. Ukubwa wa chombo cha chakula utategemea sana umri wa nguruwe unaotaka kuanza nao kufuga au ulio nao. Jedwali hapa chini kitakusaidia sana kutengeneza chombo kitakachokidhi mahitaji ya nguruwe wako.

| **Umri wa nguruwe** | **Urefu wa chombo** | **Upana wa chombo** | **Kimo cha chombo** |
|---|---|---|---|
| Nguruwe wanaonyonya | Sm 15-20 kwa nguruwe | Sm 20 | Sm 10 |
| Nguruwe wanaonenepeshwa | Sm 30-35 kwa nguruwe | Sm 20 | Sm 15-20 |
| Nguruwe wenye mimba | Sm 40-50 kwa nguruwe | Sm 35-40 | Sm 15-20 |
| Nguruwe wanaonyonyesha | Sm 40-50 kwa nguruwe | Sm 35-40 | Sm 15-20 |
| Nguruwe Dume | Sm 40-50 kwa nguruwe | Sm 35-40 | Sm 15-20 |


Vyombo vya chakula visafishwe kila siku ili kuweka chakula safi kitakacho mvutia nguruwe kula chakula. Na view na umbali wa kutosha kati ya chombo na chombo kumruhusu nguruwe kuchagua chakula anachotaka.




7. **Vyombo vya maji**

Vyombo vinavyotumika kwa chakula vyaweza pia kutumika kuwekea maji ya kunywesha nguruwe kama inavyoonekana hapa chini hasa kwa mashamba madogo.

Kwa mashamba makubwa mfumo wa bomba unaweza kutumika kwa kuingiza mabomba ya maji ndani ya nyumba ya nguruwe (automatic drinkers) na nguruwe wakanywa maji kwa muda wanaotaka wao (tazama kielelezo hapa chini).




Nguruwe wanahitaji maji safi nay a kutosha kwa siku, na mahitaji yao kulingana na umri wa nguruwe ni kama yalivyo kwenye jedwali hapa chini. Maji yanapaswa yawepo muda wote ili kumruhusu nguruwe kunywa maji kwa kadri na muda atakao yeye.

| Aina/umri ya nguruwe | Kiasi cha maji kwa siku (Lita) |
|---|---|
| Nguruwe wanao kua | 6 hadi 8 |
| Nguruwe dume | 12 hadi 15 |
| Nguruwe wenye mimba | 10 hadi 12 |
| Nguruwe wanaonyonyesha | 20 hadi 30 |

**REFERENCE:**

Food and Agriculture Organization of the United Nations (FAO). Farmer's Hand Book on Pig Production (For the small holders at village level).